

OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA HUDUMA ZA MALAZI / NYUMBA ZA KUPANGA

KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0030

MKANDARASI wa Uhandisi , Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakiaji Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika Ghuba ya Tanga, anakaribisha Makampuni kueleza nia yao kwa:

Utaji wa Huduma za Malazi

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yaliyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuo wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:

Timu ya Mradi wa BBN inahitaji huduma ya nyumba za kupanga katika JJI LA TANGA na zenye sifa zifuatazo:

- Nyumba zilizo na samani zote pamoja huduma zote zinazohitajika
- Nyumba ya Chumba 1 cha kulala, vyumba 2 vya kulala vyote vinajitegemea, ziwe nyumba za kujitegemea au kuchangia kwenye uzio mmoja,
- Nyumba ya Kawaida ya Familia yenye vyumba 3 vya kulala au vyumba 4 ziwe za kujitegemea au kwenye uzio wa kuchangia,

- Majengo yaliyosafishwa, safi na yaliyofukizwa dawa za wadudu kitaalamu
- Inapaswa ziwe Tanga mjini na kufikika kwa urahisi
- Ziwe na eneo la Maegesho & Jenereta kwa ajili ya umeme wa dhurura
- Ziwe na huduma ya Umeme na maji

KIWANGO CHA MAHITAJI:

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Hati miliki au Hati Rasmi zinazothibitisha umiliki wa mali na azimio la kukodisha mali hiyo,
- Michoro ya usanifu inayoonyesha mpango wa nyumba kwa BBN kutathmini mahitaji,
- Picha za nyumba au nafasi inayopatikana kwa BBN kutathmini pamoja na eneo, ikiwa kuna ziara
- Leseni halali ya biashara na usajili
- Pendekezo la viwango vya kodhi kwa mwezi ikiwa pamoja na viwango vya huduma, masharti ya malipo na vigezo vya kukodisha.
- Wasifu wa kampuni yenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa.
- Kwa kampuni, kufuata kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovuitwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com . (Upeo wa Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 02 Februari 2023 1800hrs Saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saina ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

Kumbuka: Kampuni zilizo hitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.